




**Reginald Mengi**
@regmengi

# WASHINDI WA SHINDANO LA NAMNA YA KUUKABILI UMASKINI 2013/2015

## Twita kwa Dk Mengi














Imeandaliwa na
Pamoma

# WASHINDI WA SHINDANO LA NAMNA YA KUUKABILI UMASKINI 2013/2015

Twita kwa Dk Mengi

Imeandaliwa na
Pamoma

Takribani jumla ya Mawazo zaidi ya 50,000 jinsi ya kukabiliana na umaskini nchini Tanzania na mawazo ya biashara yalitolewa katika kipindi cha mwaka mmoja na nusu. Na katika mawazo hayo Watanzania 97 wengi wao wakiwa vijana,waliweza kuyafanyia kazi mawazo yao na kufanya Biashara.

# YALIYOMO


1.0 **TWEETS 12 ZA DK REGINALD MENGI**........................................................ 1
1.1 Tweets Za Dk Reginald Mengi za Kuhamashisha Vijana Kupigana Na Umaskini. ........................................................................ 1
2.0 **UTANGULIZI** ............................................................................................ 3
3.0 WASHINDI WA MASHINDANO KUANZIA MEI 2013- Mei 2015 ..................5
3.1 Washindi Mei 2013 ........................................................................... 5
3.1.1 Mawazo ya Washindi wa Mei 2013 ...................................................5
3.2 Washindi wa Juni 2013 .......................................................................7
3.2.1 Mawazo ya Washindi wa Juni 2013 .................................................. 7
3.3 Washindi wa Mwezi Julai 2013 ..........................................................9
3.3.1 Mawazo ya Washindi wa Julai 2013 .................................................. 9
3.4 Washindi wa Agosti 2013 ..................................................................11
3.4.1 Mawazo ya Washindi wa Agosti 2013 .............................................. 11
3.5 Washindi wa Septemba 2013 ............................................................13
3.5.1 Mawazo ya Washindi wa Septemba 2013 .........................................13
3.6 Washindi wa Oktoba 2013 .................................................................15
3.6.1 Mawazo ya Washindi wa Oktoba 2013 .............................................. 16
3.7 Washindi wa Novemba 2013 ............................................................. 17
3.7.1 Mawazo ya Washindi wa Novemba 2013 .......................................... 18
3.8 Washindi wa Desemba 2013 .............................................................. 19
3.8.1 Mawazo ya Washindi wa Desemba 2013 ........................................... 20
3.9 Washindi wa Januari 2014 ................................................................. 21
3.9.1 Mawazo ya Washindi wa Januari 2014 .............................................. 22
3.10 Washindi wa Februari 2014 ............................................................... 23
3.10.1 Mawazo ya Washindi wa Februari 2014 ............................................ 24
3.11 Washindi wa Machi 2014 .................................................................. 25
3.11.1 Mawazo ya Washindi wa Machi 2014 ................................................ 26

3.12 Washindi wa Aprilii 2014 .................................................................. 27
3.12.1 Mawazo ya Washindi wa Aprilii 2014 ................................................... 27
3.13 Washindi wa Mei 2014 ........................................................................ 29
3.13.1 Mawazo ya Washindi wa Mei 2014 ...................................................... 29
4.0 **WASHINDI BORA WA MASHINDANO YA MIEZI JANUARI 2015- MEI 2015** ........................................................................ 30
4.1 Washindi 10 Bora wa Shindano la Mwezi Januari 2015 ......................... 30
4.2 Washindi 10 Bora wa Shindano la Mwezi Februari 2015 ...................... 31
4.3 Washindi 10 Bora wa Shindano la Mwezi Machi 2015 .......................... 32
4.4 Washindi 10 Bora wa Shindano la Mwezi Wa Aprili 2015 ..................... 33
4.5 Washindi 10 Bora wa Shindano la Mwezi Wa Mei 2015 ........................ 35
4.6 Washindi 10 Bora wa Shindano la Mwezi Wa Juni 2015 ..................... 36



**Reginald Mengi** @regmengi - July 21, 2015

There is no way Tz can realize true development if leaders lack confidence and belief in the ability&capacity of their country & its people.

# 1.0 TWEETS 12 ZA DK REGINALD MENGI

## 1.1 Tweets Kumi na Mbili Za Dk Reginald Mengi za Kuhamashisha Vijana Kupigana Na Umaskini.



*Mchango wako katika maisha ya wengine siyo lazima uwe wa fedha tu, hata ushauri unaweza kubadilisha maisha yao na ukumbukwe kwa hilo.*

*22 Julai 2013*

---



*Kuanza biashara kwanza ni lazima uwe na wazo bora la biashara unayotaka kufanya, halafu tafuta mtaji.*

*26 Sept. 2013*

---



*Una haki ya kutajirika mradi unafanya shughuli halali. Hakuna mwenye haki ya kukupimia kiasi cha utajiri halali Mungu aliokupa.*

*2 Feb. 2014*

---



*Nimekusikia ukisema huwezi sababu huna uwezo. Badilika! Inua mkono wako wa kulia juu, sema kwa sauti kubwa NITAWEZA NIKIWEZESHWA.*

*15 Feb. 2014*

---



*Tz ina rasilimali nyingi, zikitumika vizuri kijana mwenye ndoto ya kutajirika akifanyia kazi ndoto yake na kuwezeshwa anaweza kuwa bilionea.*

*29 Juni 2014*

---



*Nasikia umeshindwa kuanza biashara sababu umekosa fedha. Lakini una mtaji mkubwa usio wa kifedha, kama 1) wazo bora 2) nguvu yako.*

*25 Julai 2014*

---



*Age is just a number. Umri mdogo au mkubwa kamwe usiwe kisingizio cha kutoanza biashara.*

*25 Julai 2014*

---



*Wazo bora la biashara ni mali. Lilinde. Ukishindwa kuliendeleza mwenyewe mtafute mbia(partner) mfanye pamoja.*

*27 Julai 2014*

---



*Ushauri wangu kwa vijana...kamwe msiwaamini sana wanasiasa. Watawatumia kama C..m na watawatupa kama taka wakishatimiza malengo yao.*

*Agosti 9 2014*

---



*Kijana kumbuka neno "Asante" ni muhimu na la kiungwana katika maisha yako. Eti umekwishampa Mungu asante kwa mema aliyokutendea jana?*

*Agosti 19 2014*

---



*Kijana kumbuka huwezi kuwa mfanyabiashara mkubwa na maarufu bila kukopa. Kama unaogopa kukopa basi sahau ndoto ya kuwa mfanyabiashara mkubwa.*

*Machi 4 2015*

---



*Kijana kama unataka kufanikiwa kibiashara na uwe mfanyabiashara mkubwa lazima unyenyekevu, uaminifu & kusema kweli viwe sehemu ya mtaji wako.*

*Juni 2 2015*

## 2.0 UTANGULIZI

Tarehe 13 Mei 2013, Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk Reginald Mengi, aliandika kwenye akaunti yake ya twita (@regmengi), hivi: "Umaskini umekuwa sugu. Kwa mwaka mmoja (1) kuanzia mwezi Mei nitatoa Shmilioni 1 kila mwezi kwa tweet nitakayochagua kuwa bora kushinda vita na umaskini"

Kuanzia mwezi Juni, 2013, shindano lilibadilika kidogo kwa Dk. Mengi kutuma swali linalohusiana na jinsi ambavyo Mtanzania anaweza kujijenga kiuchumi au jinsi wadau mbalimbali wanavyoweza kuwezesha watu kujijenga kiuchumi, ambalo washiriki walitakiwa kulitafutia jibu bunifu. Kila mwezi, mawazo yaliyokuwa yanapokewa yalichaguliwa na jopo la majaji likiongozwa na Dk. Donath R. Olomi wa Institute of Management and Entrepreneurship Development (IMED) – Taasisi ya Uongozi na Ujasiriamali. Mawazo yote mazuri yalichaguliwa. Baada ya hapo yakawa yanachaguliwa mawazo 10 bora zaidi ambayo yalitangazwa kila mwezi na Dk. Mengi. Katika haya 10 yalichaguliwa mawazo matatu bora zaidi, ambayo yalipewa zawadi.

Katika kipindi cha miezi 12 yalitolewa jumla ya mawazo 13,635. Baadaye Dk. Mengi aliongeza mwezi mmoja wa fainali ambapo aliwataka washiriki waeleze jinsi walivyotumia wazo walilolitoa au walililoliona kwenye tweet kujijenga kiuchumi. Hivyo basi, mwezi wa mwisho ulikuwa unataka kuonyesha utekelezaji wa mawazo bunifu.

Mwaka 2015, Dk Mengi alizindua Shindano la Wazo la Biashara kwa kifupi 3N, ikiwa ni kifupisho cha 'Nitabuni wazo la biashara, Nitatekeleza, na Nitafanikiwa' kuanzia Januari 8, 2015 hadi Juni 30, 2015. Shindano hili liliandaliwa kwa lengo la kushawishi wajasiriamali wa Tanzania kuyafanyia kazi mawazo yao na kuibuka na biashara zenye tija. Shindano likawa linamtoa mshindi mmoja kila mwezi. Katika kipindi cha miezi 6 ya shindano hili, jumla ya mawazo 36,857 yalitolewa. Jedwali hapa chini linaonyesha jumla ya mawazo yaliyotolewa katika kila mwezi tangu Mwezi Mei 2013 hadi Juni 2015(miezi 19).

| S/N | Mwezi na Mwaka | Jumla ya tweets (mawazo) |
|---|---|---|
| 1 | Mei 2013 | 400 |
| 2 | Juni 2013 | 1,510 |
| 3 | Julai 2013 | 919 |
| 4 | Agosti 2013 | 979 |
| 5 | Septemba 2013 | 643 |
| 6 | Oktoba 2013 | 414 |
| 7 | Novemba 2013 | 1,542 |
| 8 | Desemba 2013 | 553 |
| 9 | Januari 2014 | 1,280 |
| 10 | Februari 2014 | 978 |
| 11 | Machi 2014 | 1,935 |
| 12 | Aprilii 2014 | 940 |
| 13 | Mei 2014 | 1,542 |
| 14 | Januari 2015 | 1,680 |
| 15 | Februari 2015 | 5,096 |
| 16 | Machi 2015 | 9,437 |
| 17 | Aprilii 2015 | 6,500 |
| 18 | Mei 2015 | 6,800 |
| 19 | Juni 2015 | 7,344 |
| **Jumla** | | **50,492** |

Vigezo vitatu muhimu vilivyotumika katika kuchagua mawazo bora ni;

1). Wazo linaloeleweka na kuelezeka kirahisi
2). Wazo bunifu – kuwe na upya fulani katika wazo
3). Wazo liwe linawezekana kutekelezwa katika mazingira ya Tanzania

# 3.0 WASHINDI WA MASHINDANO KUANZIA MEI 2013- Mei 2015

## 3.1 Washindi Mei 2013

Dk. Mengi amewapongeza washindi na kutoa zawadi kwa washindi wafuatao:
@Jillwithyou- Jilly Kyomo
@ngugulu – Peter George
@Donludovick- Ludovick Angelino

### *3.1.1 Mawazo ya Washindi wa Mei 2013*

***1). Wazo la @Jillwithyou- Jilly Kyomo***

Tuwe na utamaduni wa kupenda kile tukifanyacho, kukifanya kwa moyo, uadilifu, heshima na kujali muda, hata kama umejiajiri.

***Dk Olomi:*** Sababu ya kuchagua hili wazo ni kwamba, kila mmoja wetu anaweza kufanya hivi, na ukweli ni kwamba ukifanya hivi popote ulipo si rahisi ukawa au ukaendelea kuwa maskini. Watu wengine wanafikiri mafanikio yanakuja kwa kufanya mambo ya ajabu, lakini kwa uelewa na uzoefu wangu, sina shaka kwamba ukifanya chochote kile ufanyacho, iwe nyumbani, shuleni, kwa mwajiri au kwenye biashara yako kwa kukipenda, kwa moyo, kwa uadilifu, kwa heshima na kwa kujali muda, si rahisi ukabaki maskini.

***2). Wazo la @ngugulu – Peter George***

Kuweka mfuko wa mikopo kwa vijana wanaowekeza kwenye kilimo na kukuza sekta ya kilimo na viwanda vyenye uhusiano wa moja kwa moja.

***Dk Olomi:*** Rasilimali mojawapo inayoweza kutumika kuzalisha ajira nyingi kwa vijana wanaotoka vyuoni na mashuleni ni ardhi, hivyo nakubaliana kuwa tukiwa na njia za kuwezesha vijana kuingia huko itasaidia sana kupunguza umaskini. Lakini tunahitaji mawazo (tweets) bunifu zaidi yanayoonyesha ni kwa jinsi gani hili wazo linawezekana, maana mikopo peke yake haitoshi kuwafanya vijana wajiajiri kwa njia endelevu kwenye kilimo.

***3). Wazo la @Donludovick***

Uoga ndio chanzo cha umaskini, tunauchekea ufisadi, tunashindwa kuchagua na kuteua watu sahihi wa kutuongoza.

***Dk Olomi :*** Ni ukweli kuwa umaskini unachangiwa sana na ufisadi na ukosefu wa uongozi bora katika ngazi mbalimbali, na sisi kama jamii hatujatekeleza wajibu wetu wa kuupiga vita ufisadi na kuchagua viongozi wazuri. Natumaini tutaendelea kupata tweets juu ya njia bunifu za jamii kupambana na ufisadi na kupata viongozi bora bila kuvunja sheria au kufanya vurugu.



*Washindi wa Mwezi Mei wakipongezwa na kupewa zawadi na Dk. Mengi.*

## 3.2 Washindi wa Juni 2013

Dk. Mengi aliwapongeza washindi na kutoa zawadi kwa washindi wafuataao:
@ ekombe45 –Keith Kombe
@ kai_mollel
@WillfredTarimo

### *3.2.1 Mawazo ya Washindi wa Juni 2013*

#### *1). Wazo la @ ekombe45 – Keith Kombe*

Ili kufanikiwa kiuchumi katika mazingira yoyote unahitaji maandalizi. Kama serikali haijakuandalia, usiendelee kusubiri. Jiandalie.

***Dk Olomi:*** Sababu ya kuchagua wazo hili ni kuwa kama kila mtu akitambua kuwa ana wajibu wa kwanza kujiandalia misingi ya mafanikio, atatumia fursa yoyote iliyopo, hata kama ni ndogo kujijenga, na hakika umaskini ataukwepa. Wako watu wengi sana wanafikiri kuwa ustawi wao utaletwa na serikali, au wazazi, au wadau wengine.

#### *2). Wazo la Kai Mollel*

Nina wazo ambalo naamini litasaidia kiasi kikubwa sekta ya elimu na jamii....unaonaje mkianzisha programu ya wanafunzi kujitolea (students volunteer programs).

***Dk Olomi:*** Sababu ya kuchagua wazo hili ni kuwa kama kila mtu akitambua kuwa ana wajibu wa kwanza kujiandalia misingi ya mafanikio, atatumia fursa yoyote iliyopo, hata kama ni ndogo kujijenga, na hakika umaskini ataukwepa. Wako watu wengi sana wanafikiri kuwa ustawi wao utaletwa na serikali, au wazazi, au wadau wengine.



*Washindi wa Mwezi Juni wakipongezwa na kupewa zawadi na Dk. Mengi.*

***3). Wazo la @WillfredTarimo Wilfred Tarimo***

Tujiajiri kifikra kwanza kabla ya kujiajiri kiuhalisia. Kujiajiri kifikra ni kuweka MTAJI wa Mawazo ndani yako, mawazo ya UBUNIFU.

***Dk Olomi:*** Hili wazo lilituvutia kwa sababu kila jambo huanzia kwenye dhamira, ambayo hutokana na fikra au mtizamo. Imani na nia ya kujitegemea au kuwa tegemezi inatoka ndani ya moyo wa mtu. Watu wanaoshindwa kuanza kujiajiri huwa wameshajiambia kwamba hawawezi kwa sababu hii au ile. Wale wanaojiajiri wanaamua kufanya hivyo, halafu wanatafuta njia ya kufanikisha azma yao.

## 3.3 Washindi wa Mwezi Julai 2013

Swali la kushindania la Mwezi Julai: Je Kijana asiyekuwa na ajira wala fedha anawezaje kujijenga kiuchumi?

Wafuatao ni washindi bora wa Mwezi Julai 2013, nao walikuwa ni;

@tonyakir -Tony K
@johnmkungu- John Mkungu
@mtangazajim- Maduhu

### *3.3.1 Mawazo ya Washindi wa Julai 2013*

**1). *Wazo la @tonyakir -Tony K***

Kama kijana fikiria katika hali uliyopo ni nini unachoweza kuifanyia jamii yako, ukipata jibu huo ndio mtaji na ajira yako.

***Dk. Olomi:*** Ukiangalia wazo hili lina maudhui yanayofanana na yale yaliyoshika nafasi ya tatu na ya pili. Lakini wazo hili limebeba maana kubwa zaidi, na ndiyo maana limepata ushindi wa kwanza. Tony anasema kwamba popote kijana alipo, asijali kwamba hana fedha wala ajira. Aangalie ni nini anachoweza kuifanyia jamii inayomzunguka, na akishapata jibu, huo ndio mtaji na ajira yake. Tumevutiwa sana na usemi huu. Kijana yeyote ambaye atakuwa na mtazamo ulioainishwa kwenye wazo hili, hakika hatapata shida. Kuanzia sasa ukisikia kijana anayesema hana kazi hivyo hafanyi chochote, mpe wazo hili, apate mahali pa kuanzia. Tutaomba Tony aelezee zaidi wazo hili.

**2). *Wazo la @johnmkungu- John Mkungu***

Kijana atambue fursa anayoipenda na kuimudu, aanze kuhudumia watu kwa kujitolea, ubora wa huduma yake ukijulikana watu watamtafuta kwa malipo.


***Dk Olomi:*** Yako mawazo mengi yaliyotolewa yanayohusiana na kijana kuanza kufanya kazi kwa kujitolea ili watu waone uwezo wake na hivyo kumwajiri. Lakini hili limechaguliwa kwa sababu linaongeza ubora kwa kusema kuwa kijana achague kazi ya kujitolea anayoipenda na kuimudu, na aifanye kwa ubora. Vijana wengi wanaotafuta ajira

hawafahamu kwamba watu wengine wakijua unachoweza kufanya inakuongezea nafasi kubwa sana ya kupata ajira nzuri.

***3). Wazo la @mtangazajim – Maduhu***

Kama kijana yuko kijijini anaweza kulima na kuuza mazao akaweka akiba, na kama yuko mjini anatafuta vibarua, anaweza kuweka akiba na kuwa mjasiriamali.

***Dk Olomi:*** Yako mawazo mengi yaliyotolewa yanayofanana na hili. Wazo hili limechaguliwa kwa sababu linaelezea kwa ufupi na ufasaha mfano wa njia rahisi anayoweza kupita kijana asiyekuwa na ajira wala kipato kuanza safari ya kujijenga kiuchumi, na pia linatoa mfano wa aliyeko kijijini na aliyeko mjini. Baadhi ya watu wenye uwezo mkubwa kiuchumi leo walianza kama vibarua au wakulima kama Maduhu alivyoeleza.



*Washindi wa Mwezi Julai wakipongezwa na kupewa zawadi na Dk. Mengi.*

## 3.4 Washindi wa Agosti 2013

Swali la Mwezi Agosti: Nini kifanyike kuzalisha ajira nyingi kwa vijana hapa Tanzania?

Wafuatao ni washindi bora wa Mwezi Agosti 2013:

@LilianWilson21- Lilian Wilson,
@SuzanaSenga - Susan Senga,
@OmbeniKaaya - Ombeni Kaaya

### *3.4.1 Mawazo ya Washindi wa Agosti 2013*

**1). *Wazo la @LilianWilson21***

Wajasiriamali waliofanikiwa pamoja na serikali waanzishe mifuko ya kuwekeza mitaji kwenye biashara za vijana zenye uwezekano wa kukua haraka, badala ya kutegemea mikopo ya benki au taasisi ndogo za fedha.

***Dk Olomi:*** Uwekezaji kwa njia ya hisa (venture capital) huenda pamoja na kutoa ushauri na kumuunganisha mwanzilishi wa biashara na mitandao na fursa mbalimbali.

Sababu ya kuchagua wazo hili ni kwamba utaratibu wa kuanzisha uwekezaji kwa njia ya hisa (venture capital) ukiweza kutumika kwenye miradi ya vijana utasaidia kupatikana kwa fedha isiyokuwa na riba wala kuhitajika kurejeshwa haraka, na hapohapo vijana wenye hizo biashara kupata ushauri kutoka kwa wajasiriamali weledi na wazoefu. Hii inaweza kuchangia kujenga kampuni nyingi zinazokua haraka, ambazo nazo zitakuza ajira kwa vijana wengine.

**2). *Wazo la @SuzanaSenga***

Kuanzishwe vipindi maalum kutoa elimu ya ujasiriamali ya kuwawezesha vijana kuwatoa katika fikra ya kuishi kutegemea ajira ili kujiajiri.

***Dk Olomi:*** Sababu ya kuchagua wazo hili ni kwamba elimu na weledi ni nguzo kuu katika kupata ajira na kujiajiri. Tatizo lililoko ni kwamba elimu nzuri inayotolewa nje ya shule na vyuo ni gharama kubwa, na ni vijana wachache wana

uwezo wa kuilipia. Kukiwa na utaratibu wa kutoa elimu inayojenga uwezo wa vijana kujiajiri na kuajirika kwa njia ya vipindi maalumu kupitia vyombo ya habari, kunaweza kusaidia sana upatikanaji wa ajira.

***3). Wazo la @OmbeniKaaya***

Tafiti wanazofanya wanafunzi wa elimu ya juu mwaka wa mwisho ziwe zinahusu jinsi ambavyo watakavyojiajiri katika fani zao: Itasaidia wengi wajiajiri.

***Dk Olomi:*** Wazo hili limechaguliwa kwa sababu iwapo kila mwanafunzi atalazimika kufanya utafiti wa jinsi anavyoweza kujiajiri anapokuwa chuoni, hii itamfanya aone fursa zilizoko ambazo anaweza kuzitumia kujiajiri. Inaweza kusaidia baadhi ya wale ambao hawaoni nini cha kufanya baada ya kumaliza chuo kutambua kitu wanachoweza kufanya. Hata kama wengine wataanza kwa kuajiriwa, wanaweza baadaye kurudi kuanza shughuli walizozipanga wakiwa kwenye ajira au wakishaziacha na zikachangia upatikanaji wa ajira.




*Washindi wa Mwezi Agosti wakipongezwa na kupewa zawadi na Dk. Mengi*

## 3.5 Washindi wa Septemba 2013

Swali la Mwezi Septemba 2013: Rasilimali za nchi hii zinawezaje kutumika kuongeza ajira kwa vijana?

Washindi wa shindano hili ni:

@gkiwango -Godfrey Kiwango,
@OmbeniKaaya- Ombeni Kaaya
@Julius_Shirima- Julius James Shirima

### *3.5.1 Mawazo ya Washindi wa Septemba 2013*

#### *1). Wazo la @gkiwango*

Vyuo vya kilimo vifundishe kwa vitendo, viwapatie vijana wanaosoma mashamba kwa mikopo huku wakiendelea kusoma.

***Dk Olomi:*** Sababu ya kuchagua wazo hili ni kwamba mojawapo ya raslimali kubwa tuliyonayo na ambayo haijatumika vizuri kuzalisha ajira ni ardhi. Pia tuna vyuo vingi vya kilimo. Hata hivyo elimu ya kilimo na ufugaji haitolewi kwa namna ya kuwaandaa wahitimu kuwa wakulima au wafugaji, bali kuwa maofisa. Utaratibu uliopendekezwa ukitumika utaleta mapinduzi makubwa katika elimu na kusaidia wahitimu wa masomo hayo kujiajiri na kuajiri wengine katika kilimo. Pia itasaidia kuondoa kasumba iliyojengeka kwamba kilimo si ajira nzuri kwa vijana au wasomi.

#### *2). Wazo la @OmbeniKaaya*

Lianzishwe jarida maalum na mtandao ambapo vijana watakuwa wanapata habari za fursa mpya zitokanazo na rasilimali za Kitanzania.


***Dk Olomi:*** Sababu ya kuchagua wazo hili ni kwamba kuna fursa nyingi zinazotokana na rasilimali nyingi ambazo Tanzania imejaliwa kuwa nazo. Hata hivyo vijana wengi hawazijui au hawazioni. Likianzishwa jarida kama lilivyopendekezwa na kukawa na utaratibu wa kutoa elimu na taarifa kuhusu rasilimali zilizoko na jinsi ya kuzitumia kuzalisha ajira kwa kujiajiri

na kuajiri wengine, inaweza kuwa njia nzuri ya kuchangia matumizi ya hizo rasilimali na kuzalisha ajira. Tweets nyingi zilipendekeza kutolewa kwa ajira na taarifa. Tofauti ya hii ni kwamba pia imependekeza njia bunifu ya kufanya hivyo.

***3). Wazo la @Julius_Shirima***

Makampuni yanayochimba rasilimali za Taifa yachangie mfuko wa kuwezesha biashara na ujuzi kwa vijana.

***Dk Olomi:*** Wazo hili limechaguliwa kwa sababu njia bora zaidi ya kumuweka kijana katika nafasi ya kujiajiri au kuajiriwa ni kumjengea elimu, weledi na mtaji. Rasilimali nyingi kama madini, gesi na mafuta hazitoi ajira nyingi moja kwa moja. Pia, bila kuwa na vijana wenye ujuzi unaotakiwa, ajira nyingi katika migodi na viwanda vya gesi, mafuta, nakadhalika, zitachukuliwa na wageni. Serikali inagharamia elimu, lakini tunafahamu pia kwamba uwezo ni mdogo. Tukiweza kuunganisha mapato yatokanayo na uchimbaji wa rasilimali zetu na kujenga uwezo wa vijana kujiajiri na kuajirika itatusaidia sana. Kulikuwa na mawazo mengi yenye mwelekeo huu. Sababu ya kuchagua wazo hili ni kwamba limeelekeza njia ya kupata hayo mapato yatakayotumika. Mawazo mengi yameishia kusema kuwa faida au mapato yatumike kwa ajili hii. Pia wakati baadhi ya mawazo yamependekeza fedha hiyo itumike kama ruzuku kwa vijana, jambo ambalo si endelevu.



*Washindi wa mwezi Septemba wakiwa pamoja na Dk. Mengi baada ya kupewa zawadi.*

## 3.6 Washindi wa Oktoba 2013

Swali la tweet bora Oktoba 2013 ni: Toa mfano unavyoweza kuanzisha biashara bila kutumia fedha.

Washindi wa tweet bora Octoba 2013 ni:
@SuzanaSenga,
@migrace10,
@byevic

### *3.6.1 Mawazo ya Washindi wa Oktoba 2013*

***1). Wazo la -@ SuzanaSenga***

Unaweza kuuza wazo ukaanza biashara. Mfano, niliuza wazo la stori ikachezwa filamu na msanii maarufu nchini. Ikaniwezesha kuanzisha biashara.

***Dk Olomi:*** Tulivutiwa na hili wazo kwa sababu Suzana ametupa mfano mzuri sana wa jinsi unavyoweza kuanza safari ya kujiajiri kwa kutumia tu akili yako au kipaji ulichojaaliwa nacho. Kila mtu ana akili, na kila mtu ana kipaji au vipaji fulani. Hata kama hana fedha anaweza kutumia akili au kipaji kuanza kufanya kitu ambacho kitamjenga kiuchumi.

***2). Wazo la @migrace10***

Mfano unaweza kutafuta mtu wa kukudhamini kwa mwenye mali ili uuze kwa faida zaidi, ili baadae na wewe umiliki biashara yako.

***Dk Olomi:*** Hapa tunaona jinsi ambavyo unaweza kuanza biashara kwa kutumia mtaji wa kuaminika na hivyo kuazimwa mali za watu wengine kufanyia biashara. Wako watu wanaanza au kukuza biashara zao kwa njia hii. Wako ambao wanaweza kuwa na mtaji wa mabilioni, lakini sehemu kubwa ikawa ni mali ya watu wengine. Watanzania tujifunze kujenga mtaji wa kuaminiwa ili tusipate shida ya fedha za kufanyia au kupanulia biashara zetu.

***3). Wazo la @byevic Victor A Byemelwa***

Elimu uliyopata itumike kama mtaji wako kwa kufundisha wanafunzi wa chini yako na tumia eneo lako kama ofisi. Hapo mtaji ni elimu.

***Dk Olomi:*** Hili ni wazo ambalo mtoaji amekuwa akilifanyia kazi. Kwa kutumia elimu yake, huwafundisha walioko nyuma yake kwa kuwatoza malipo kidogo. Ni njia nyingine ya kutumia akili au elimu kama mtaji.



*Washindi wa Mwezi Oktoba wakipongezwa na kupewa zawadi na Dk. Mengi.*

## 3.7 Washindi wa Novemba 2013

Swali la Mwezi Novemba ni: Wananchi wa kawaida wanaweza kushirikishwaje kwenye uchumi wa gesi asilia?

Washindi wa Tweet bora Novemba ni:

@byevic- Victor A Byemelwa
@SSagatik- Shadrack Sagati
@davie bless- Davie Bless

### *3.7.1 Mawazo ya Washindi wa Novemba 2013*

***1). Wazo la @byevic***

Kupewa elimu ya kuitambua gesi, fursa zitokanazo na gesi pamoja na wazawa kupewa fursa ya kumiliki vitalu kama mali yetu Watanzania.

***Dk Olomi:*** Hakuna jambo kubwa kuliko elimu ya kuwawezesha watu kutambua na kutumia fursa zilizoko kwenye sekta yoyote ikiwemo gesi. Pia ili gesi iwanufaishe Watanzania, ni muhimu waweze kufaidika na kumiliki na kuichimba gesi yenyewe, na si tu kusema wasubiri kufaidika kwenye makandokando ya mlolongo wa hiyo gesi. Thamani kubwa na faida kubwa kwenye madini na mafuta iko kwenye bidhaa yenyewe.

***2). Wazo la @SSagatik***

Wananchi wenye uwezo waunde umoja ili waweze kuchangishana fedha wapate mtaji na Serikali iwapatie vitalu kupitia umoja wao.

***Dk Olomi:*** Ni kweli kwamba uwekezaji kwenye gesi unahitaji mitaji mikubwa. Na ni ukweli kwamba wako Watanzania wenye uwezo wa kukusanya nguvu zao na kuanzisha kampuni ambazo zinamilikishwa na kutafuta wabia kuwekeza kwenye utafiti na uchimbaji wa gesi.

***3). Wazo la @daviebless***

Kwenye uchumi wa gesi kuna kazi nyingi ambazo zinaweza kufanywa na mzawa, mfano: kusambaza vyakula, maji, hakuna haja wapewe wageni.

***Dk Olomi:*** Uchumi wa gesi unafungua fursa nyingi ambazo zinaweza kuchangia sana kukuza kipato cha Watanzania, kwani kutahitajika mazao, vifaa na huduma mbalimbali katika uchimbaji, usindikaji, na usambazaji wa gesi. Watanzania wakijiandaa vizuri wanaweza kufaidika na haya yote.



*Washindi wa Mwezi Septemba wakipongezwa na kupewa zawadi na Mkurugenzi wa ITV na Radio One Joyce Mhaville kwa niaba ya Dk Reginald Mengi.*

## 3.8 Washindi wa Desemba 2013

Swali la tweet la Desemba 2013 ni: Fursa gani za kujijenga kiuchumi ambazo watu wengi hawazioni?

Washindi bora wa Desemba ni:

@JoyTemu -JoyDinah Goodluck
@Asslii_Ali - Ali Suleiman
@paulmushik - Paul K Mushi

### *3.8.1 Mawazo ya Washindi wa Desemba 2013*

***1). Wazo la @JoyTemu***

Kuwekeza kwenye ukuzaji wa vipaji, sanaa & ubunifu kama kuanzisha academy na kuuza matunda ya sanaa yatakayoongeza kipato.

***Dk Olomi:*** Watanzania wamejaliwa vipaji katika maeneo mbalimbali, na mpaka sasa ni sehemu ndogo sana ya vipaji hivi inaendelezwa na kutumika kibiashara. Hii inatokana na hali duni ya maisha iliyokuwepo, malezi na elimu itolewayo kutokuweza bado kutambua na kulea vipaji na kutokuwepo makampuni ya mapromota yaliyokomaa. Hii ina maana bado kuna fursa kubwa sana ya kuibua vipaji na kuviendeleza kibiashara.

***2). Wazo la @Asslii_Ali***

Ufugaji wa samaki kama kambare na sato, ufugaji huu utasaidia kuongeza kipato cha mtu mmoja mmoja na uhakika wa chakula (samaki).

***Dk Olomi:*** Samaki ni mojawapo ya mboga inayopendwa sana, na bei yake iko juu. Ufugaji wa kambale ni shughuli ambayo siyo ngumu, na kuna watu wachache wanaoifanya, ingawa kwa ufanisi mdogo kutokana na kukosa maarifa na ushauri. Kambale wanakua haraka na kwa gharama ndogo, hivyo ni eneo lenye fursa kubwa.

***3). Wazo la @paulmushik***

Fursa ya kuwekeza katika misitu kwa ajili ya ufugaji nyuki kwa biashara ya asali na miti ya mbao kwa ujenzi na matumizi mengine.

***Dk Olomi:*** Tanzania imejaliwa misitu mingi, mito mingi na ardhi kubwa ambayo ina uoto lakini haitumiki vizuri kwa kilimo. Asali ni zao linalohitajika sana kwenye soko la Tanzania na nje. Hivyo ufugaji nyuki kibiashara ni fursa kubwa sana ambayo bado haijatumiwa vizuri.



*Washindi wa Mwezi Desemba wakipongezwa na kupewa zawadi na Mkurugenzi wa ITV na Radio On Joyce Mhaville kwa niaba ya Dk Reginald Mengi.*

## 3.9 Washindi wa Januari 2014

Swali la Mwezi Januari: Ni jinsi gani Wafanyabiashara wakubwa wanaweza kuwainua wafanyabiashara wadogo?

Washindi wa Tweet bora Januari ni:

@laumasha – Mh. Lawrence (Lau) Masha
@EmmanOssie- Ossie Emman
@Mnyalapejunior - Mnyalape Junior

### 3.9.1 Mawazo ya Washindi wa Januari 2014

***1). Wazo la @laumasha***

Wafanyabiashara wakubwa watoe ushauri, wawape moyo na fursa wafanyabiashara wadogo. Serikali inatakiwa kuwajengea wote mazingira ya kufanikiwa.

***Dk Olomi:*** Wafanyabiashara wakubwa wengi walianza biashara ndogo ndogo na wana uzoefu wa kukutana na kupambana na changamoto za aina mbalimbali. Wakijitoa kusaidia wale wadogo kwa ushauri na kuwapa moyo, itasaidia sana kuwaendeleza.

***2). Wazo la @@EmmanOssie***

Kuwa na vitengo vya wafanyabiashara wakubwa ambavyo vitawasaidia wafanyabiashara wadogo kukuza biashara zao kwa kupatiwa elimu.

***Dk Olomi:*** Iwapo kila mfanyabiashara mkubwa angetenga sehemu ya utajiri wake kuwasaidia vijana wanaoanza biashara kama anavyofanya Dk. Mengi, kungekuwa na matokeo mazuri na makubwa kwa hao wafanyabiashara wadogo na kwa nchi.

***3). Wazo la @Mnyalapejunior***

Kuandaa shindano la mfanyabiashara bora ambalo litakuwa maalumu kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo kwa lengo la kuwatia moyo.

***Dk Olomi:*** Mashindano kama haya yanatoa fursa kwa watu kujifunza na kupata hamasa. Hivyo yangesaidia sana kuchochea ari na kuonyesha mifano ya mafanikio.



*Washindi wa Mwezi Januari wakipongezwa na Dk Reginald Mengi baada ya kupewa zawadi.*

## 3.10 Washindi wa Februari 2014

Swali la Mwezi Februari ni: Kwa mawazo yako ni vipi Serikali inaweza kuwawezesha wafanyabiashara wadogo?

Washindi wa Tweet bora ya Februari ni:

@byevic - Victor A Byemelwa
@GNdewario - Glory Ndewario
@Mnyalapejunior - Mnyalape Junior

### *3.10.1 Mawazo ya Washindi wa Februari 2014*

***1). Wazo la @byevic***

Ipitishwe sera katika serikali kwa manunuzi yote madogo madogo ya serikali yapewe kwa wafanyabiashara wadogo ili kukuza soko lao.

***Dk Olomi:*** Nchi nyingi zinatumia sera ya manunuzi kuwezesha biashara ndogo kupata soko na kurasimisha biashara na mifumo yao. Serikali za mitaa, serikali kuu na taasisi zake zikiweka sera madhubuti za kununua kutoka kwenye biashara ndogo itakuwa kama kuzipa biashara hizi chakula, na hivi zitakua. Hivi sasa serikali inanunua samani nyingi kutoka nje, badala ya kuwawezesha mafundi seremala wa hapa nchini. Hili jambo linahitaji kubadilishwa.

***2). Wazo la @GNdewario***

Serikali itumie kambi za JKT kutoa elimu kwa vijana jinsi ya kukuza wazo na kuwa la biashara kubwa yenye kutoa ajira na utajiri.

***Dk Olomi:*** Kambi za JKT ni fursa kubwa sana ya kujenga mtizamo, stadi na kwa ujumla weledi wa vijana. Kambi hizi zinaweza kutumika kujenga kujiamini, ufundi kwenye stadi fulani, uzoefu kwenye hiyo stadi na ujasiriamali. Inawezekana pia kambi hizi zikawezesha vijana kukaa kwa muda wa miaka 2-3 wakijizalishia na hivyo kujenga mtaji. Ni bahati mbaya kwamba kambi hizi sasa zinaonekana ni mzigo badala ya vituo vya mafunzo na uzalishaji.

***3). Wazo la @Mnyalapejunior***

Kuunda utaratibu wa kukutana na wafanyabiashara wadogo kusikiliza kero zao na kufanya maamuzi yenye tija kwao.

***Dk Olomi:*** Mojawapo ya njia inayoweza kutumika kuleta mabadiliko chanya katika biashara ndogo ni viongozi wa serikali kujenga utaratibu na utamaduni wa kukutana mara kwa mara na wafanyabiashara ili kusikiliza kero

zinazowakwaza na mawazo chanya waliyonayo ya kuendeleza uchumi katika vijiji, wilaya, miji na hata nchi. Bahati mbaya sana watumishi wengi wa serikali hawatambui kuwa wanaweza kupata mawazo mazuri sana kutoka kwa wafanyabiashara.



*Washindi wa Mwezi Februari wakipongezwa na kupewa zawadi na Mkurugenzi wa ITV na Radio One Joyce Mhaville kwa niaba ya Dk Reginald Mengi.*

## 3.11 Washindi wa Machi 2014

Swali la Mwezi Machi ni: Toa mfano wa jinsi kitu kinachokera watu wengi kinavyoweza kugeuzwa kuwa fursa ya biashara.

Washindi wa tweet bora ni:

@gnyaissa - Gerald Nyaissa
@GNdewario -Glory Ndewario
@PolycarpMramba

### *3.11.1 Mawazo ya Washindi wa Machi 2014*

***1). Wazo la @gnyaissa***

Mikoa ya Dodoma na Iringa ina upepo mkali mpaka kero! Tuanzishe miradi ya kufua nishati ya umeme kwa kutumia upepo.

***Dk Olomi:*** Nchi hii ina utajiri wa vyanzo vya nishati ambavyo sasa hivi vinachukuliwa kama kero, ikiwemo upepo mkali. Ingawa kuna mawazo na mipango ya kutumia upepo kuzalisha umeme, bado halijafanyika sehemu nyingi au kwa kiasi kikubwa.

***2). Wazo la @GNdewario***

Kero ya misongamano katika miji na sehemu za manunuzi, unaweza kuanzisha biashara ya kufanya manunuzi kwa niaba ya watu kwa malipo.

***Dk Olomi:*** Ni kweli kabisa kwamba kila kero inayomkabili mtu inakuwa ni fursa kwa mwingine, na msongamano wa magari unaleta fursa nyingi, ikiwemo hii iliyotajwa.

***3). Wazo la @PolycarpMramba***

Ukataji miti misituni kwa ajili ya kuni, mkaa na matumizi mengine ni kero unaweza kutafuta mbegu za miti upande kisha uuze kwa bei nafuu.

***Dk Olomi:*** Ukataji miti msituni ni tatizo kubwa la kimazingira, na mtu anaweza kupanda miti inayokuwa haraka au kwa muda mrefu kupata kuni na mahitaji mengine.



*Washindi wa Mwezi Machi wakipongezwa na kupewa zawadi na Dk. Mengi.*

## 3.12 Washindi wa Aprili 2014

Swali la tweet la Mwezi Aprilii ni: Mzazi afanye nini kumwandaa mtoto kufanikiwa kiuchumi?

Washindi wa Tweet bora kwa mwezi Aprilii ni:

@abnerymwogelaya
@samsonshilla - shilla Samson
@gnyaissa

### *3.12.1 Mawazo ya Washindi wa Aprili 2014*

#### *1). Wazo la @abnerymwogelaya*

Mzazi amuandae mwanae kuishi kwa kujiamini, kuthubutu, kuanza kufanya kitu cha kumuinua kiuchumi anachodhani ni vyema akifanye kwa wakati huo.

***Dk Olomi:*** Mtoto atakayeandaliwa namna hii si rahisi kuja kushindwa kujitegemea katika maisha yake.

***2). Wazo la @samsonshilla***

Mzazi amwandae mtoto katika mambo makuu manne; elimu, kupenda kufanya kazi kwa bidii, ubunifu na kupenda kumcha Mungu.

***Dk Olomi:*** Mtoto aliyeandaliwa hivi pia atafanikiwa. Ni vizuri kwamba ameongeza kumcha Mungu.

***3). Wazo la @gnyaissa***

Kila siku mzazi mnong`oneze mwanae; "Mungu amewapa matajiri saa 24 kwa siku sawa na anavyokupa wewe, tumia saa hizo kwa faida".

***Dk Olomi:*** Hii ni kweli kabisa. Tajiri na maskini muda walionao ni ule ule. Tofauti ni jinsi wanavyoutumia.



*Washindi wa Mwezi Aprilii wakipongezwa na kupewa zawadi na Dk. Mengi.*

## 3.13 Washindi wa Mei 2014

Swali la tweet la mwezi Mei 2014 lilikuwa ni: Eleza jinsi ulivyotumia au utakavyotumia wazo ulilotoa au lililotolewa na mwingine katika shindano la tweet na Dk Mengi kujijenga kiuchumi?

Washindi wa Tweet bora kwa mwezi Mei ni:

@BLuwanja,
@DepoLevelTZ
@freddyfabby

### *3.13.1 Mawazo ya Washindi wa Mei 2014*

***1). Wazo la @BLuwanja -Baraka Luwanja***

Kwa elimu niliyoipata imenisaidia katika kufunga kifaa cha kupimia uelekeo wa nguvu ya upepo (wind vane) kwa ajili ya kuzalisha umeme utokanao na nguvu ya upepo kuvutia maji ardhini na kuyauza imenikwamua na nimeajiri watu watatu.

***Dk Olomi:*** Hii tweet ilituvutia sana kwa kuwa mtoaji wazo aliona kwenye shindano akaamua kulifanyia kazi katika mazingira yake, na pia ameweza kuajiri watu watatu.

***2.). Wazo la @DepoLevelTZ -Deo Polycarp***

Wazo la Ubunifu, elimu na vipaji. Nimetengeneza mtambo unaotumia nishati asilia kutotoa na kutunza vifaranga halafu nauza/natunza kwa ujira.

***Dk Olomi:*** Mtambo asilia kutotoa vifaranga. Deo Pia amefuatilia shindano akapata wazo la kufuga vifaranga na amebuni njia isiyokuwa na gharama ya kutotoa vifaranga.

***3). Wazo la @freddyfabby-Freddy Fabby***

Wazo la kuimarisha uwekezaji wa ndani, umenifanya nibuni mradi wa kiwanda cha kukamua mafuta ya alizeti eneo lenye wakulima wa zao hilo.

***Dk Olomi:*** Freddy pia alipoona umuhimu wa kuimarisha uwekezaji wa ndani amepata wazo la kuwekeza kwenye kiwanda kidogo na kulitekeleza.

# 4.0 WASHINDI BORA WA MASHINDANO YA MIEZI JANUARI 2015 - MEI 2015

Mashindano ya Mwaka 2015 ( Januari –Juni) Dk. Mengi ametoa zawadi kwa mshindi wa kwanza na wengine 9 waliomfuata.Aidha waliofungana mawazo waligawana zawadi.

## 4.1 Washindi 10 Bora wa Shindano la Mwezi Januari 2015

Mshindi wa kwanza Mwezi Januari 2015: @shayo_fredrick alielezea mpango wa kutengeneza mafriji mabovu na kuyageuza yatumike kuwa mashine bora zenye uwezo wa kutumika kuangulia vifaranga vya kuku kwa wafugaji. (Incubators).

Washindi wengine ni:

1). **Wazo la Jesse Temba@Jestemba:** Nitabuni mradi wa kununua madeni sugu kwa bei ya chini na kutumia ujuzi wangu wa sheria kuyadai kwa kufuata sheria za nchi.

2). **Wazo la Charles @kapondo:** Kuanzisha kiwanda kidogo cha kutengeneza toothpicks na berbacue sticks. Hakuna kiwanda kama hicho nchini Tanzania.

3). **Wazo la George Rashid@george_rashid:** Kuanzisha kampuni itakayokuwa inakopesha vitendea kazi vya biashara kwa wajasiriamali wadogo ambao wana ujuzi na wanahitaji vifaa.

4). **Wazo la Otaigo Elisha@otaigiE:** Weed management business, the services will be provided to farmers using modern agriculture technology.

5). **Wazo la Aphonce Mallya, MBA@aAlphoncemallya:** Plastic garbage recycling by converting plastic waste into building planks to replace timber/wood for roofing furniture, road signs.

6). **Wazo la Japhet Bachu@japhetbachu:** Cage fish farming in Lake Victoria e.g. tilapia, catfish, value addition through fillet processing, packaging & supplying.

7). **Wazo la Kibanga@SirikibangaOmari:** Shule za kata hazina mradi hata wa kununua vitafunwa kwa walimu, nitafuga nao kuku, tutauza na kugawana faida.

8). **Wazo la Emmanuel Buberwa@EmmanuelBuberwa:** Nitafungua kampuni itakayowezesha kupatikana usafiri wa uhakika na haraka kwa kushare pamoja na taxi/private car kupitia simu ya mkononi.

9). **Wazo la Gerald Nyaissaa@gnyaissa:** Mahoteli na migahawa mingi nchini haina wasambazaji wa mboga. Nimeanzisha kilimo cha mboga PWANI, nitasindika na kuwa msambazaji bora.

## 4.2 Washindi 10 Bora wa Shindano la Mwezi Februari 2015

Mshindi wa kwanza Mwezi Februari 2015: Viana Mulokozi@Vianamulokozi ametoa wazo la kuwatafutia wanafunzi wa vyuo nafasi za field (mafunzo) kwenye makampuni kupitia internet kwa kutumia online system.

Washindi wengine ni:

1). **Wazo la Frank Mwasekaga@kaggga:** Mwezi uliopita nilizindua mradi uitwao LinkUp, unaowawezesha wanafunzi wote katika vyuo vikuu nchni kupokea habari za masuala yote yanayovihusu vyuo vikuu.

2). **Wazo la @Vianamulokozi:** Kuwatafutia wanafunzi wa vyuo nafasi za field (mafunzo) kwenye makampuni kupitia internet kwa kutumia online system.

3). **Wazo la Michael Emmanuel @michaelemmanue2 :** Kuuza kwa kutumia mtandao na kufikisha bidhaa kwa wateja hasa wafanyakazi katika Jiji la Dar Es Salaam kutegemea na mahitaji yao.

4). **Wazo la Fanuel @fanuelmbonde92:** Kuwa na mtandao wa bajaji ambao utamuwezesha mteja kupiga simu kituoni na kuletewa bajaji sehemu alipo.

5). **Wazo la Mjameica Rapstar @MjameicaRapstar:** Nitauza madini kwa njia ya mtandao,ambapo nitayanunua kutoka kwa wachimbaji

wadogo wadogo na kuyaprocess,nitatumia website kuuza.

6). **Wazo la Nedson Kashaija @nedson17:** Kuanzisha kampuni ya kutengeneza filter za maji majumbani kwa kutumia vitu vya asili kupunguza kunywa maji machafu ktk familia.

7). **Malamba Jerald @jerald_malamba:** Kampuni ya kisheria ya kufuatilia na kuadhibu watupa takataka ovyo jijini Mwanza. Kosa moja gharama ni sh. 1000. Wateja wapo mno.

8). **Wazo la Sashaknowles @sasha_knowless:** Kuanzisha kampuni itakayojishughulisha na majanga au maafa itakayokuwa inasaidia watu na taasisi mbalimbali/kampuni katika mambo hayo.

9). **Wazo la Wazo la Nyahbinghi @Wabuela :** Wazo langu #2 la biashara ni 'huduma ya vyoo kwa abiria safarini.

10). **Wazo la Kibanga @SirKibangaOmari:** Kuanzisha saluni za kunyolea nywele zinazotembea mitaani.(MOBILE barber shops) Nitanunua mini hiace ya kubeba viti na vifaa vingine vya salon. Mteja atapiga simu then anafuatwa alipo.

## 4.3 Washindi 10 Bora wa Shindano la Mwezi Machi 2015

Mshindi wa kwanza Mwezi Machi 2015 ni **Bukhary Kibonajoro @Kibonajoro** aliyefikiria kutengeneza "online accounting software called StraightBook targeting 3.1Mil SME to manage their businesses & they pay monthly".

Washindi wengine ni:

1). **Wazo la Salim said @electronicsalim:** Nitaunda chaja ya simu(inatumia nishati itokanayo na mwendo wa baskeli) itumike wakati unaendesha baskeli yako(SOKOkanda ya ziwa).

2). **Wazo la Harrykageyo @Harrykageyo:** Wazo la kuanzisha mfumo wa mitandao badala ya kwenda kulipia ulipaji safari za mikoani kwa bus physically.

3). **Wazo la Abdallah Mdira @ABDALLAHMDIRA:** Project is about a home security system in which a cell phone will alert the owner of the house when an intruder enters the house.

4). **Wazo la Victor A Byemelwa @byevic:** Wahitimu wengi wa JKT hukosa kiunganishi cha kupata ajira. Nitaanzisha kituo cha kuunganisha wahitimu.

5). **Wazo la norman billy @normanbillynth:** For global market i will have ICLN ONLINE LIBRARY DATABASE where through internet clients can access our services worldwide.

6). **Wazo la atumulikye E isaac @ABenhag:** Nitafungua parcel transportation agency kwa kuweka mikataba na wamiliki wa mabasi, nitaanza na mikoa ya DAR ES SALAAM, SINGIDA,ARUSHA,DODOMA,MWANZA.

7). **Wazo la Stephen Benard Maswe @MasweStephen:** Kukusanya, kuboresha na kuchapisha kazi za fasihi simulizi (Hadithi)katika vijitabu vidogo vitakavyowalenga zaidi watoto.

8). **Wazo la Irene Enock @irene_enock:** TTo create a system called EMPLOY ME where by employees will put their CV's. It will be easy for employers to get qualified people.

9). **Wazo la JOYCE PATRICK TANO @joycetano:** To develop an Online and Phone Apps database of all Hotels and lodges to enable customer lodge and pay online.

## 4.4 Washindi 10 Bora wa Shindano la Mwezi wa Aprili 2015

Mshindi wa Mwezi Aprilii 2015 ni **DAUD M.** @GodOpenDoor na **ANTHONY MHANDA** @ANTHONYMHANDA:

**Wazo la DAUD M. @GodOpenDoor** ni kuanzisha mfumo wa ulinzi shirikishi kupitia simu za mkononi, wanajamii tutaunganishwa katika njia moja itakayo-alert uhalifu ukitokea.

**Wazo la ANTHONY MHANDA @ANTHONYMHANDA:** kujenga maabara ndogo ya kuchakata na kupima ubora wa Asali ya Wafugaji na wasindikaji mkoani Katavi.

Washindi wengine ni:

1). **Wazo la la Philemon Naman @philynaman:** I will use GPS tech to make SmartDkive software yenye taarifa kuhusu road such as speed zones to make them comply with limits.

2). **Wazo la kataraihya@dafrosakatays** ni kuanzisha ka kiwanda ka kutengeneza aluminium lunch boxes huku Tanzania maana zilizopo zote niimported.

3). **Wazo la salehe senkondo @0_senkondo:** opening software"JIPIME".i will collect past paper exams secondary student will do examination online and making their work online.

4). **DavidDee @GodIsMyBase:** kutumia residues plastics kutengeneza MOVABLE FISH SWAMP.Inasaidia kufuga samak ht kwny nyumba ya kupanga sababu inahamishika.

5). **Freddy Freddy @Freddy_fabby:** nimetengeneza mashine inayopasua mawe na kusawazisha viwanja hapa Magulilwa, wananchi wanaikodi, nategemea kutengeneza nyingi zaidi.

6). **Deodatus P. Mramba @IamDeoMramba:** Nimebuni mabegi kwa ajili ya wanafunzi yenye tochi & solar panel juu ya begi, inajichaji anapotembea juani kwa ajili ya kusomea usiku.

7). **Mbonea mpembeni @mpembeni:** To create a platform website where people can design their own t-shirts online, and I will print and sell to them.

8). **Yusuph maglah @yusuphmaglah:** Nitaanzisha kambi ya kuhudumia vilivyo wanaoishi mitaani na kuwatafutia ajira/fursa za kazi, huduma italipiwa kwa njia mbadala.

## 4.5 Washindi 10 Bora wa Shindano la Mwezi wa Mei 2015

Washindi wa Mwezi Mei 2015 ni OMBENY SANGA @OMBENYS na @ KelvinLaswai.

**Wazo la OMBENY SANGA @OMBENYS:** Kutengeneza kifaa maalum "boxpedia" kinachofundisha kama mwalimu, ninatengeneza mwenyewe,na kina ufanisi mkubwa.

Wazo la Kelvin Laswai: Nimegundua BioLite Stoves.Ni Jiko Jipya Lenye Consumption Ndogo Ya Kuni Na Sehemu Kucharge Simu Na Redio. Nitayauza Hapa Nchini.

Washindi wengine ni:

1). **Wazo la Francisca Fabian @Nascacisca:** Dietary food delivery service many people are busy and can't afford time to prepare for dietary food,delivering to them is helpful.

2). **Wazo la Juma Malekani @juma_malekani:** AC nazotengeneza kwa kutumia feni,zinaleta ubaridi kama wa AC zenyewe,hazili umeme,nitafundisha wengine.

3). **Wazo la Massaga Massaga @igungakwetu:** Mota itazungushwa na engine wakati wa kusaga na umeme utazalishwa.

4). **Wazo la Raymond Jofrey @kusongwa:** I have developed a healthy snack from a crop grown by smallholder farmers.The product is good for school children and mothers.

5). **Wazo la Glory G @glory1_2:** Restaurant&Bar that sell fast food&alcohol 24 hours and late night delivery services, so you can buy at night.

6). **Wazo la ibrahim enock @IbrahimEnock:** 3N. i establish an app for farmers to register to get their subsidies, 500tshs voucher per year. and 50tshs charge per month.

7). **Wazo la Daud Maganda @DaudMaganda:** I've made a device to extinguish fire, It is capable of detecting fire and start to extinguish automatically, IT IS COMPLETE.

8). **Wazo la balelazo mtondo @HMtondo:** Wazo langu Nitasindika samaki kwa njia ya asili na kuwasambaza majumbani, hoteli na supermarket kwa njia ya mtandao.

## 4.6 Washindi 10 Bora wa Shindano la Mwezi Wa Juni 2015

Washindi ni:

1). **Wazo la Goodluck M. Temu @MrGoodluckTemu:** Nimetumia tairi za gari zisizotumika kubuni round table kwa kuisukia ukili/napaka rangi pembeni & kioo juu halafu naiuza kwa bei nafuu.

2). **Wazo la Daniel @EntrepreneuralQ:** I will establish MOBILE FARM LABORATORY to help farmers to measure their farm soil before Cultivation.Tshs, 15,000 per acre.

3). **Wazo la The Geek @mlawishe_jay Jun 21:** I have designed a FINANCIAL TUTOR,a software targeting the Tanzanian SACCOSSES in boosting their financial productivity.

4). **Wazo la God Ngarumia @SirNgarumia Jun 13:** Nimebuni portable table kwa kutumia mabox makubwa yasiyotumika kwa ajili ya wanafunzi hasawa vijijini wasio na madarasa/madawati.

5). **Wazo la Zahra @mvikilwa:** Nitafundisha elimu ya maisha kwa wanafunzi mashuleni kuondoa low self-esteem kwa vijana na kutoza ada kidogo.

6). **Wazo la OnesmoMgaya @IbrahimOnesmo:** I develop a web-based system that networks embassies globally 4 recruiting & teaching non-native Swahili foreigners @ pays $17 @ 1h.

7). **Wazo la asifiwemkane @mkane_asifiwe:** Wazo langu ni kutengeneza sabuni za kuoshea majokofu na kukata harufu mbaya.

8). **Wazo la Jamilaharoubjuma@HaroubJuma:** tutengeneze generator inayotumia mvuke badala ya mafuta na generator ya upepo na sensor kuwasha taa kwa rimoti.

9). **Wazo la Marco ThobiasNtobi @mikentobi:** Aim to provide cheap, affordable, cost-saving lighting supplement (Bottle Bulb) at day/ nighttime to many unprivileged individuals.

10). **AlbogastAmani M @AlbogastAman** yeye ameeleza namna ya kutengeza na kuuza kifaa kinachoweza kupokea na kugawa umeme kutoka kwenye mita kati ya wapangaji katika nyumba/ vyumba vya kupanga.

# Reginald Mengi

Tweets **Photos** Favorites

















